VIAPO VYA UBATIZO

1

- Unakubali Biblia kama neno lenye pumzi ya Mungu, na unalichukua kama mwongozo wako wa imani na matendo?
  2 Timotheo 3:16, 17; Matendo ya Mitume 20:32

2

- Unaamini kuwa Kristo ni mwana wa Mungu wa milele na mwokozi wa wanadamu?
- Umemkubali kama mwokozi wako kibinafsi wa ukombozi kutoka kwa dhambi, ambao Huupeana kupitia kwa neema Yake?
- Utamualika yeye kila siku kuishi moyoni mwako kupitia kwa Roho Mtakatifu?
  Yohana 1:12-13; Wagalatia 2:20

3

- Umetubu, na kukiri dhambi zote kwa Mungu unazozijua, ukiamini kuwa Yeye, kwa minajili ya Kristo amekusamehe?
- Jinsi iwezekanavyo, umefanya upatanisho na wale ambao umewakosea au na wale ambao wamekukosea?
  1 Yohana 1:9; Mathayo 5:23-26; Ezekiel 33:15.

4

- Unaamini kuwa Roho Mtakatifu ni tofauti na ana utu kivyake; kwamba ndiye Mtu wa Tatu katika Uungu, pamoja na Baba na Mwana?
- Ni lengo lako kuishi maisha yaliyosalimishwa kwa Mungu, kufanya nia Yake, na kutunza amri Zake, kupitia kwa nguvu ya Roho Mtakatifu?
  Warumi 12:1; Wakolosai 3:17; Ufunuo 12:17; 22:14; Yohana 14:15-18.

5

- Utanuia kudumisha ushirika na Mungu kwa ibada ya kibinafsi kwa maombi na kuchunguza Biblia?
- Utaunga au kufanya ibada ya familia, asubuhi na jioni, nyumbani mwako?
  Danieli 6:10; 1 Timotheo 2:1; 2 Timotheo 2:15.

6

- Unatambua wajibu wako kibinafsi kuwapa waziwazi wengine Injili ya Milele?
- Utajikabidi, kwa ushahidi na mfano, kuwaongoza wengine kusalimisha maisha yao kwa Kristo.
- Unaamini kuwa Injili ya Milele inayofaa kupeanwa ni Ujumbe wa Malaika Watatu wa Ufunuo 14, na kuwa ujumbe huu wa Ujumbe huu wa Injili unafaa kupeanwa kwanza kwa kanisa la Masalio la Mungu kabla ya Sheria ya Jumapili, katika hatua mbili; ikifuatiwa na dunia, baada ya Sheria ya Jumapili?
- Ukiwa umeukubali Ujumbe huu wa Injili, unaamini kuwa tumewajibishwa kuenda na kupeana Kilio Kikuu cha Malaika wa Tatu; kuwaita waume na wake watoke Babeli na kuingia katika kanisa ka Mungu la Masalio?
- Unaamini kuwa chini ya nguvu za mvua ya masika - ambayo ni kumwagwa kwa Roho Mtakatifu - wale ambao hukubali Ujumbe wa Injili kwa kweli watatakaswa kabla ya Kufungwa kwa Rehema, wala sio baadaa yake?
  Mathayo 28:19; Marko 16:15, Ufunuo 14:6-14; 18:1-4; Yoeli 2:28; Hosea 10:12

7

- Unaaamini kwa Marejeo ya karibu ya Yesu Kristo; na kuwa kuja kwake kutakuwa binafsi, kunakoonekana, kunakosikika, na ataandamana na malaika wake wote wa mbinguni?
  Matendo 1:9-11; 1 Wathesalonike 4:16-17; Yohana 14:1-3.

8

- Unaamini kuwa mwanadamu ni wa kufa; na katika mauti yuko katika hali asiyojitambua, inayoashiriwa kwa pumzi ya Mungu kama kulala?
- Unaamini kuwa katika Marejeo ya Pili ya Yesu Kristo, waaminifu wa wa vizazi vyote watafufuliwa, wakutwe juu, na kupewa kutokufa pamoja na wateule walio hai kukutana na Bwana angani?
  Danieli 12:2; 1 Wathesalonike 4:13-16; 1 Wakorintho 15:51-55.

9

- Ukitambua kwamba utiifu kutoka kwa moyo, na wala sio kwa akili tu, ni tunda la Roho Mtakatifu, na ukiwa umeingia katika maisha ya kutakaswa, unaamini kuwa Amri Kumi ndizo nakala ya tabia ya Mungu, na kwamba kupenda kuzitunza, kupitia kwa nguvu za Roho Mtakatifu, ni ushahidi wa wokovu kwa wateule?
  Ufunuo 22:14; 14:12; 12:17; Yuda 24; 1 Wakorintho 10:13.

10

- Unaamini kuwa uongofu ndiyo uzoefu wa kuzaliwa upya?
- Unaamini kuwa hadi uzaliwe kwanza kwa Roho (ambao ni ubatizo wa toba; msamaha na kuhesabiwa haki; na wa utiifu na kutakaswa), ukifuatiwa na kuzaliwa kwa maji (ambao ni ubatizo kwa kuzamishwa, na tamko la uzao huu mpya), kwamba huwezi kuingia katika Ufalme wa Mungu?
- Unaamini kuwa kuhesabiwa haki sio tu kazi ya Kristo kusamehe makosa yetu yaliyopita, bali pia ni uwezo wa kuishi sasa bila dhambi katika mwili huu wa kufa?
  Yohana 3:3-5; Warumi 6:7; 1 Petro 1:22-23; 1 Yohana 4:5-10.

11

- Unaamini ujumbe mkuu wa Kristo ni Haki yetu; kwamba tunapaswa kuhesabiwa haki na kutakaswa, na karibu mbeleni kutukuzwa, pekee kupitia kwa kafara Yake na huduma ya Ukuhani Mkuu kwetu?
  Warumi 5:1-9; Matendo 26:18; Waefeso 5:25-27.

12

- Mwanadamu hakuubwa tu kwa sura ya Mungu, aliumbwa awe Mwenzake. Lakini shetani amefanya kazi kuiharibu sura ile na kuiweka yake kwetu, kwa hivyo kumfanya mwanadamu kuwa mwenzake. Kwa hivyo amefanikiwa kuharibu mpango wa kimungu katika uumbaji wa mwanadamu.
- Mpango wa wokovu ni mbinu ya Mungu ya kumrejesha mwanadamu kutoka kwa utumwa wa dhambi, kwa kuirejesha sura ya Mungu katika mwanadamu na kumrudisha katika utiifu wa Mungu. Ni wa ajabu katika unyenyekevu na ukamilifu wake, kwa maana haipatiani msamaha kamilifu pekee, bali pia kwa urejesho wetu kamilifu.
- Mbinu ambayo ukombozi huu ulifanya ni Kristo kuja Ulimwenguni katika mwili wenye dhambi unaofanana na wetu, ambao ndani yake aliunganisha uungu na ubinadamu. Licha ya kuja katika mwili wa dhambi ulioanguka, alikuwa tofauti na wenye dhambi, kwa maana ubinadamu aliouchukua ni usiokuwa na dhambi. Ulikuwa sawa na wenye uwiano mzuri, unaofanana na wa Adamu kabla ya anguko. Asili yake ya ubinadamu haungeweza, na wala haungetenda dhambi, ili mradi ulikuwa umeunganishwa na uungu, ndio uliuokuwa chanzo cha nguvu Yake.
- Unaamini kuwa mfano aliotuachia alipokuwa hapa ulimwenguni hufanya uwezekano wetu wa kuunganisha ubinadamu wetu na uungu wake, na hivyo basi kuishi maisha ya ushindi, hata maisha ya imani, wakati tuko katika mwili sawa ulionajisiwa ambao alikuwa nao alipokuwa hapa duniani?
  Warumi 8:3; 2 Wakorinto 5:21; Waebreania 4:15; 7:26; 10:5; Zaburi 40:7-9; 1 Petro 2:22; 1 Yohana 3:5, 9.
  Review and Herald, March 10, 1891 par. 6; Review and Herald, June 18, 1895 par. 2; Review and Herald, July 17, 1900 par. 8; Review and Herald, December 24, 1901 par. 1; Signs of the Times, April 3, 1884 par. 8; Signs of the Times , October 25, 1905 par. 1-2; Testimonies for the Church, volume 7, 29.2; Te Desire of Ages, 363.1; Te Great Controversy, 506.1; Manuscript Releases Volume 17, 26.3; Manuscript Releases Volume 18, 221.2; Leter 83, 1905; Medical Ministry, 181.3

13

- Unaamini kuwa siku ya saba ya juma ni siku takatifu ya Mungu ya Sabato; siku ya pumziko kutoka kwa harakati za kidunia; siku ya ibada ya kipekee kwa Mungu?
- Unaelewa kuwa Sabato huanza Ijumaa jua linapotua na kwamba maandalizi yote yanapaswa kufanywa kabla ya wakati huo, ili kuanza Sabato na ibada ya kufungua?
- Unaelewa kwamba inatamatika Jumamosi jua linapotua, na inapaswa kutamatishwa na ibada ya kufunga ya shukrani?
  Luka 23:56; Kutoka 20:8-11; Isaya 58:13-14

- Unaitambua kwamba Sabato; kama ukumbusho wa uumbaji., inawakilisha muhuri wa Mungu, na kwamba ibada ya Jumapili ni bandia ya kipagani inayoelezwa katika Biblia kama "Alama ya Mnyama"?
  Kutoka 31:13; Ezekieli 20:12, 20; Ufunuo 13:16; 14:1, 9, 10; Mwanzo 2:1-3.

14

- Unatambua kwamba Upapa ndio Mpinga Kristo mkuu wa unabii wa Biblia; na ndio uliokuwa nguvu kubwa ya kutesa ya zama za giza; na tena utawatesa wateule wa Mungu mwisho wa wakati?
- Unaamini kuwa ulijaribu kubadili sheria ya Mungu na Sabato, na umeleta makosa mengi katika kanisa la Kikristo?
- Unaelewa kuwa kama "BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA" dini zote za "kiprotestanti", isipokuwa masalio wa Mungu walioteuliwa - kanisa la Waadventista wasabato, yamerudi kwake, na kwa hivyo ni sehemu ya Babeli?
  1 Yohana 4:2-3; Danieli 7:25; Ufunuo 13:1-8; 17:5.

15

- Unakubali kwamba kanisa la Mungu liko katika hali ya Laodekia na limegonjeka kutoka kwa nyayo hadi kwa kichwa; japo limefadhaika na kasoro jinsi lilivyo, na likiwa limekubali makosa ya Kipapa, sio na halijawahi kuwa sehemu ya Babeli?
  Isaya 1:4-6; Ufunuo 13:14-8; 17:5; The Acts of Apostles 12.1.

16

- Utajaribu mpango wa Biblia kwa msaada wa kazi ya Mungu, kwa kumrudishia Zaka; moja kwa kumi ya mapato yako yote?
- Pamoja na hilo, utampa Bwana sadaka ya kafara jinsi ambavyo amekufanikisha?
- Ni lengo lako kusaidia harakati hii ambayo imeinuliwa na kuteuliwa na Mungu kupeana ujumbe wa Mwisho wa onyo kwa ulimwengu, na kupeana msaada wako wote kusaidia harakati hii?
  Walawi 27:32; Hesabu 18:20-24; 1Wakorintho 9:8-14: Malaki 3:6-12;

17

- Ni lengo lako kutii maagizo ya Mungu kula na kukunywa kwa utukufu wake kwa kuepuka kutoka kwa vinywaji vikali; tumbaku katika hali zake zote; vyakula vilivyoungwa sana; kemikali zenye chachu; kula nyama, chafu na isiyo chafu; ukiepuka vyakula vitokavyo kwa wanyama kama mayai na maziwa; nakotiki katika hali zake zote ikiwemo chai, kahawa, vinywaji vya cola; opiates; na vitu vyote vya hatari?
  1 Wakorintho 10:31; 3:16-17; Walawi 11; Mithali 23:29-30; Isaya 66:15, 17.

18

- Umenuia kufuata kanuni ya Maandiko ya adabu katika mavazi yako?
- Katika kutunza kanuni hiyo, utajitenga na muundo wowote wa vazi ambao uko nje ya kutunza kanuni hii Biblia ya adabu?
- Umenuia pia kufuata kanuni ya unyenyekevu na afya katika vazi lako?
- Utajitenga na kuvaa vipodozi; kupanga rangi makucha, na vito vya aina zote?
- Utajitahidi kufanya ushawishi wako uwe ambao unaashiria kujipamba kwa ndani, sio kwa nje; maisha ambayo yatawavutia watu kwa Kristo na sio kwako?
  1 Timotheo 2:9-10; 1 Petro 3:3-4; Kutoka 33:5-6; Mwanzo 35:2-4; Kumbukubu la Torati 22:5; Isaya 3:16-24.

19

- Kutambua umuhimu wa wito wa Kristo kwa maisha yako, ni lengo lako kujitenga na raha za dunia na matendo ya dhambi, kama vile; densi; kucheza kadi; michezo ya bodi na video; theater au sinema; kusoma riwaya; kutazama au kushiriki michezo ya ushindani; kutazamu vipindi vya televisheni visivyo vya manufaa; kusikiza nyimbo za kidunia; kutumia mtandao isivyofaa; na kuacha raha za wasiwasi?
  1 Yohana 2:15; Yakobo 1:27; 4:4.

20

- Unakubali ushauri ulio kwenye Maandiko lakini hasa katika Roho ya Unabii kutoishi mijini?
- Katika kuchagua mahali pa kuweka makazi unakubali kwamba eneo lisilo jaa na watu, iliyojitenga, mashambani, ni ya kupendelewa kuliko iliyojengwa kupita kiasi?
- Ni nia yako, na lengo lako kuacha kuishi mijini kwa minajili ya sehemu iliyojitenga mbali na shughuli mingi na mivuto iliyo mara nyingi mijini?
  Mwanzo 13:8-18; Mathayo 24:15-18; Mark 13:14-16; Luka 21:20-21; Country Living.

21

- Unaamini kuwa Yesu ndiye Kuhani wetu Mkuu; kwamba Yuko katika Hekalu la Mbinguni, akihudumu kwa ajili yetu?
- Unaamini kuwa Octoba 22, 1844, Aliianza hukumu ya upelelezi katika sehemu ya pili ya hekalu la mbinguni?
- Unaamini kuwa Yeye sasa yuko katika Mahali Patakatifu Mno, akifanya upatanisho wa mwisho wa dhambi zetu, pale ambapo hatimaye zitafutiliwa mbali, ikiwa utatubu na kuziacha?
- Unaamini kuwa hukumu ilianza na Wafu katika Kristo Octoba 22, 1844,vna kisha kuanza kwa wateule walio hai September 11, 2001?
  Danieli 8:14; 7:9-14, 25-27; Walawi 16; Matendo 3:19; Luke 21:29-32; Isaya 27:6-9

22

- Unatambua kuwa kanisa la Mungu la masalio limepewa roho ya unabii?
- Kwamba katika siku hizi za mwisho kipawa hiki kimeweza kwa kipekee kuonekana katika kanisa kupitia kwa maandiko na huduma ya Ellen Gould White?
- Kwamba maandiko yake hayana kosa na yana asili na tabia sawa na Biblia?
  Ufunuo 12:17; 19:10.

23

- Unaamini kwa, na umekubali, ibada za unyenyekevu (kuosha miguu) na meza ya Bwana; ambayo inaashiria kufa kwa nafsi, maisha ya utumishi kwa wengine, na kukabidi upya maisha yako yote kwa Kristo?
- Ni lengo lako kutembea katika nyayo za Yesu, kwa kushiriki ibada hizi?
  ` *Yohana 13:10-17; 1 Wakorinto 11:23-33; 1 Yohana 2:6*

24

- Unaamini kuwa Septemba 11, 2001 Malaika yule Mkuu wa Ufunuo kumi na nane alishuka kiunabii, hivyo ikionyesha kuanza kwa hukumu ya walio hai na kutiwa muhuri kwa wale alfu mia moja na arobaini na nne?
- Unaamini kuwa wakati huo huo Mvua ya Masika ilianza kunyunyiza juu ya Kuhani wa Kiadventista ikiwaita kulisafisha Hekalu la Bwana?
- Unaamini vile vile kuwa wakati huo huo Ole wa tatu, jinsi ulivyowakilishwa na Islamu yenye itikadi kali, ulikuja katika historia?
  Ufunuo 7; Ezekiel 9; Ufunuo 18; Matendo 3:19-21; 1 Petro 2:2-10; Ufunuo 9.

25

- Ili kuuhubiri kwa kweli Ujumbe wa Malaika wa Tatu, unaamini kuwa ni muhimu kuchunguza Biblia kutumia mbinu sawa jinsi Waanzilishi walifanya? Na kwamba mbinu hiyo iko wazi katika kanuni kumi na nne za William Miller za kuchunguza na kuielewa Biblia?
- Unaelewa kuwa mbinu hii inahitaji mashahidi wawili ili kwamba ukweli uwezi kukubalika na hutuhitaji kuligawanya Neno la Kweli kwa kutumia (application) mstari mmoja wa unabii juu ya mistari mingine sawa ya unabii?
  Isaya 28:9-13; 2 Timotheo 2:15; Mwanzo 41:32; Kumbukumbu la Torati 17:6

26.

- Unakubali misingi ya imani ya Wa-adventista Wasabato jinsi ilivyofunzwa na Waanzilishi wake, na ilivyo kwenye chati ya 1843 na 1850, na unatamani kuungana na mwili wa waumini hawa?
- Kama ushuhuda wa uamuzi huu, unaamini ubatizo kwa kuzamishwa, na ni nia yako kuonyesha imani na kukubali katika neema inayookoa ya Bwana Yesu Kristo kwa ubatizo wa wazi katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?
  Mathayo 3:6-17; 28:18-20; Wakolosai 2:12; Warumi 6:3-5; Habakkuki 2:1-3.